

102/3

**KISWAHILI
KARATASI YA TATU
(FASIH)
JULAI/AGOSTI, 2014
MUDA: SAA: 2½**

**MTIHANI WA MWIGO – WILAYA YA KIHARU/KAHURO
KIDATO CHA NNE - 2014**

**Hari Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA TATU
FASIH
MUDA: SAA: 2½**

MAAGIZO:

1. Jibu maswali **manne** pekee.
2. Swalii la **kwanza** ni la **lazima**.
3. Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki:
Yaani: **Tamthilia, Ushairi, Hadithi Fupi** na **Fasihi Simulizi**.
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu **moja**.
5. Kila swalii lina alama **20**.
6. Mtihini huu alama **80**.

SEHEMU YA A:

SWALI LA LAZIMA:

KEN WALIBORA: KIDAGAA KIMEMWOZEA

1. “Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenyewe kichaa kama yeye?”
- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
 - (b) Eleza tamathali mbili zilizotumika katika dondo hili. (alama 4)
 - (c) Thibitisha kuwa anayerejelewa ni mwendawazimu na vilevile si mwendawazimu. (alama 12)

SEHEMU YA B:

MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE

Jibu swali la 2 au 3

2. “... naona bado ule utundu wa utotoni haukukutoka. Naona unajaribu kutia kidole chako katika mzinga wa nyuki. Ni hatari!”
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
 - (b) Onyesha mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondo hili. (alama 2)
 - (c) Fafanua mnenewa alivyojibu kitisho alichotishwa katika dondo hili. (alama 10)
 - (d) “Naona unajaribu kutia kidole chako katika mzinga wa nyuki. Ni hatari.” Onyesha hatari hii inavyotokea katika tamthilia hii. (alama 4)
3. Fafanua aina zozote kumi za migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)

SEHEMU YA C:

4. USHAIRI

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayo fuata.

1. Sema semea wajiba, mwenye kutetema,
Sema na walo karibu, mbali ukisema,
Sema kufunza wajibu, noleji, hekima,
Sema ajue fulani, usihulu sema.
2. Sema yanayokukaa, yanokusakama,
Sema yaliyozagaa, kwa mbwako mtima,
Sema unajihadaa, kwani tawafuma?
Sema wajue ni nani, usiache sema.
3. Sema yote si uasi, si tengé si nomá,
Sema toa wasiwasi, upate salama,
Sema japo ni risasi, longa litauma,
Sema yote hadharani, radidia sema.
4. Sema pasi na ukali, mwiza taloloma,
Sema neno la asali ‘taramba’ kitema,
Sema kwa mzo akili, watakushituma,
Sema kwa yako maghani, usikome sema.
5. Sema zitaje ghururi, duniya ni dema,
Sema ana maghubari, duniya ni rima,
Sema duniya hatari, mwina wa nakama,
Sema sema kwa yakini, masa ghaya sema.
6. Sema ‘Kwani hamuoni, waloachwa nyuma?’
Sema pasi taraghani, uliyoyasema,
Sema wachuma tumboni, ja minyoo sema,
Sema sema mwafulani, u salama sema.

Maswali

- (a) Toa mfano miwili ya idhini ya kishairi katika shairi hili. (alama 2)
- (b) Tambua bahari zozote **nne** zinazopatikana katika shairi hili na utoe sababu. (alama 4)
- (c) Onyesha vile shaha alivyofua dafu katika kutumia mbinu zifuatazo:
(i) Anafora.
(ii) Usambamba wa kiusawe. (alama 2)
- (d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
- (e) Ujumbe wa nafsineni unamlenga nani? (alama 2)
- (f) Eleza sifa za kiarudhi katika ubeti wa **pili**. (alama 4)
- (g) Andika ubeti wa **tano** katika lugha tutumbi/nathari. (alama 4)

SEHEMU YA D:

**KEN WALIBORA NA S. A. MOHAMED
DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

Jibu swali la 5 au 6.

5. Kwa kurejela hadithi zozote tano katika Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine, Jadili jinsi maudhui ya ubaguzi yanavyofafanuliwa. (alama 20)
6. “Hapa huingii bila kuninyooshea mkono,” yule bwana akamwambia.
“Dadangu hatoki kwetu vivi hivi.”
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
 - (b) Eleza tamathali **mbili** zilizotumika katika kauli hii. (alama 4)
 - (c) Jadili uhusiano wa msemewa na maudhui yoyote **sita** katika hadithi hii. (alama 12)

SEHEMU YA E:

FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 7 au 8

7. (a) Eleza maana ya miviga. (alama 2)
- (b) Eleza dhima ya miviga katika jamii. (alama 8)
- (c) Miviga huambatana na sifa kadha. Fafanua zozote **sita**. (alama 6)
- (d) Fafanua hasara **nne** za miviga. (alama 4)

AU

8. (a) Maigizo ni nini? (alama 2)
- (b) Eleza sifa **nne** za maigizo. (alama 4)
- (c) Taja aina **mbili** kuu za maigizo. (alama 2)
- (d) Taja na ueleze sifa za mwigizaji. (alama 12)